

ATHARI ZA UWIANO WA SHERIA ZA MBEGU KWA MIFUMO YA MBEGU INAOSIMAMIWA NA WAKULIMA (FMSS) NA KWA WAKULIMA WADOGO

Uwiano wa sheria za mbegu zinathamini mbegu zilizotengenezwa kwa ajili ya kilimo cha viwanda au biashara ndani ya kanda maalum. Sheria hizi zinawanyima wakulima wadogo fursa na msaada kushughulikia aina ya kilimo kama vile kilimo cha asili au kilimo ekolojia ndani ya kanda.



Uwiano wa sheria za mbegu hazitengi vifungu kwa ajili ya mifumo ya mbegu inayosimamiwa na wakulima (FMSS) na aina ya mbegu zinazozalishwa na wakulima. Hii inaweza kuathiri kwa kiasi kikubwa aina ya mbegu za asili za wakulima ndani ya kanda, ambazo tayari zimeashanza kutoweka.

Uwiano huu utatengeneza soko kubwa la mbegu kikanda na kuathiri kampuni za mbegu zilizopo ndani ya nchi, hivyo kuongeza ueneaji wa mbegu zilizoboreshwa na kuthibitishwa. Hii inamaana kwamba wakulima wadogo watalazimika kununua mbegu zilizoboreshwa kwa bei ghali, msimu baada ya msimu.

Uwiano wa sheria za mbegu hairuhusu wakulima wadogo kuuza au kubadilishana mbegu zilizohifadhiwa shambani na aina ya mbegu za asili katika mipaka ya nchi kadhaa ndani ya kanda. Wakulima wanaweza kukumbana na tatizo kubwa iwapo watasafirisha mbegu walizobadilishana kwenye mipaka bila kibali. Hata hivyo, uwiano wa sheria za mbegu hazipigi marufuku makampuni ya binafsi kuiba taarifa za asili na mbegu kutoka kwa wakulima wa ndani ili kutengeneza aina za mbegu zilizoboreshwa, ambazo wanaweza kuwauzia tena wakulima kwa gharama ya juu.

